# Wavamizi Kwala wapewa onyo

**Pwani.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka waliovamia eneo la kuhifadhi na kuiangalia mifugo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi kwa muda, kuondoka katika eneo hilo kwa hiari la sivyo nguvu zitatumika.

Waziri Ndaki alitoa wito huo juzi alipotembelea eneo la karantini ya Kwala wilayani Chalinze, Pwani.

"Hili eneo lina maslahi ya kitaifa hivyo wananchi walioingia na kukaa huku bila utaratibu wowote, tuwaambie waondoke kwa hiari, wale tutakaowakuta tutakapoanza ujenzi wa karantini ya kisasa, tutatumia nguvu," alisema Waziri Ndaki. **(Mwandishi Wetu)**

Scanned with CamScanner

# Ofisa mifugo afariki usingizini

**Na Samson Chacha,**
TARIME

OFISA Mifugo wa Halmashauri ya Mji Tarime, Pedas Masungwa, aliyetarajiwa kustaafu mwakani, amefariki dunia akiwa usingizini.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntovya, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho kilichotokea Desemba 27, mwaka huu.

"Halmashauri yetu tumepata pigo kwa kumpoteza mtumishi mwenzetu Pedas usiku wa kuamkia Jumatatu, na taarifa za madaktari zinaeleza kuwa kifo chake kilitokana na shinikizo la damu (BP)," alisema.

Kwa mujibu wa Ntovya, familia yake ilisema Pedas alifika nyumbani kwake usiku na kwenda kulala, lakini baadaye alisikika akikoroma kwa sauti hali iliyomfanya mke wake na watoto kwenda kumwamsha bila mafanikio.

Alisema familia hiyo ilibidi iombe msaada kwa majirani kumpeleka hospitali, lakini alikuwa ameshapoteza maisha.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, mwili wa marehemu unatarajiwa kuzikwa kijijini kwake Musoma, mkoani Mara.

"Masungwa alikuwa mzalendo alijituma kwa kazi yake ya kuhudumia mifugo hata katika minada aliwahudumia wananchi, wafugaji kwa kutoa elimu kwa vitendo," alisema.

Scanned with CamScanner

# Ofisa Mifugo Tarime akutwa amefariki

**Na SAMSON CHACHA,** *Tarime*

OFISA Mifugo wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Pedas Masungwa, amekutwa amefariki nyumbani kwake.

Taarifa za kifo cha ofisa hiyo, zilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Tarime, Gimbana Ntovya, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kifo hicho kilichotokea usiku wa kuamkia jana.

"Halmashauri ya Mji Tarime imepata pigo, baada kutokea taarifa za kifo cha Pedas Kabuche Masungwa, aliyekuwa Ofisa Mifugo wa halmashauri kwa muda mrefu,"alisema.

Aliongeza kuwa Masungwa alikuwa pia akikaimu ukurugenzi mara kadhaa, ambapo alikutwa na mauti usiku nyumbani kwake akiwa amelala, akitokea kujumuika na marafiki zake kumalizia sikukuu ya Krismas.

Kwa mujibu wa Ntovya, taarifa za madaktari zinaeleza kuwa Kifo chake kimetokana na

shinikizo la damu.

Alisema kwa upande wa familia yake, inadai ofisa huyo alifika nyumbani usiku na kwenda kulala na baadaye alisikika akikoroma kwa sauti na

ndipo mke wake na watoto walijaribu kuwaita majirani na kumpeleka hospitali, ambako ilibainika alikuwa ameshafariki dunia.

Alisema mipango ya mazishi itatangazwa na familia.

"Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake peponi," alimwombea.

Wakazi wa Mji Tarime na wafanyabiashara wa mifugo wakiwemo Matiko Simon, Mzee Rugumba na Samwel Chomete, waliofika katika msiba huo walimwelezea Masungwa kuwa alikuwa mzalendo, alijituma kwa kazi yake ya kuhudumia mifugo hata katika minada aliwahudumia wananchi na wafugaji kwa kutoa elimu na kwa vitendo.

Scanned with CamScanner

UZO



Tarime
fariki

ne

uri ya Mji wa
, amekutwa

hiyo, zilitolewa
almashauri

**MUFTI** wa Tanzania, Sheikh Mkuu,Abubakar Zubeir (kulia) akimkabidhi Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, tuzo ya kutambua mchango wake kwa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) wakati wa Maulidi ya Mtume Muhammad (SAW) yaliyofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Mkuranga mkoani Pwani, juzi. (Picha na Scolastica Msewa).

Scanned with CamScanner